**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 14 April, 2007**

**Waliohudhuria**
Abdallah Khatib
Elaine Baker
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd
Kibwana Mohammad Msiga
Paulo Atibu
Shukuru Hassan

**Mgeni**
Prosper, AALOCOM

**Wanachama wapya**
Ilitangazwa kuwepo kwa wanachama wapya wane,akiwemo Jumanne aliyekuwepo kwenye mkutano,aliyekarabati baiskeli ya tairi tatu, hivyo kila mtu alijitambulisha.

**Maguta na Mikokoteni**
Elaine aliripoti kuhusu maguta (baiskeli za tairi tatu zitumikazo kusafirishia mizigo) wiki iliyopita tarehe 4aprili, manispaa ya Ilala ilitangaza kukataza uwepo wa maguta kama moja ya mikakati yake ya kuondoa msongamano katikakati ya jiji na Kariakoo. Mejah alimfahamisha Elaine na walizungumza kwa simu ,na alhamisi ilikuwa mkutano wa dharura kwa Elaine,Shukuru na Juma ili kufuatilia jambo hili. Waliandika barua kwa manispaa na mambo muhimu yalikua yafuatayo:

- Baiskeli ni njia mojawapo inayokidhi mahitaji ya usafiri mijini na zile za tairi tatu ni njia muhimu kwa ubebaji wa mzigo jijini.
- Sababu iliyotolewa na manispaa haijitoshelezi,kukatazaa uwepo wa maguta inamaanisha usafiri wa pick-up na malori uongezwe ili kikidhi mahitaji,hii itazidisha msongamano barabarani.
- Sera hii haiendani na mkakati wa Serikali wa kupunguza umaskini,kwani itondoa chanzo cha mapato kwa wengi maana wengi wanatumia maguta na mikokoteni kujitafutia kipato jijini.

Jumamosi Elaine, Abdallah, Juma, Malitika, Paulo, Shukuru na Sosthenes walitumia siku nzima kupita maeneo kam Kariakoo, Mabibo, Manzese na Tandale kukusanya maoni kutoka kwa watumiaji wa mikokotni na maguta na sahihi ili kupinga sera ya manispaa.
Zaidi ya sahihi mia nne zilikusanywa siku hiyo, Abdallah na Paulo waliendelea siku iliyofuata na idadi kuu ya sahihi zilizokusanywa zilikuwa 835.

Jumanne Juma alikwenda kwenye ofisi ya Meya Ilala kufuatia miadi na tuliambiwa kurudi alhamisi asubuhi. Alhamisi asubuhi Elaine, Juma, Paulo na Shukuru walikwenda ofisini hapo na kugundua kwamba manispaa ilitangaza mkutano pia Kariakoo, hivyo watumia mikokoteni karibu mia mbili walikuwepo pia. Kumi kutoka UWABA na wengine walizungumzia matatizo ambayo yangesababishwa na sera hii ya manispaa kwa watumiaji wa maguta na mikokoteni, maduka, na wenye vibanda sokoni wanaohitaji kusafirisha bidhaa kwa maguta na mikokoteni,na msongamano wa malori na pick-ups katikati ya jiji. Meya alisema kuwa yeye hawezi kutoa maaamuzi ya mwisho na anahitaji kuwasiliana na wanakamati wa baraza na angewaelezea kuhusu tuliyoongea na kutuita tena kutufahamisha maamuzi yao.

Kulikuwa na waandishi wa habari, na wanachama wa UWABA walioneshwa kwenye Television ya Chanel 10, na jioni hiyo kulikuwa na picha kwenye gazeti la Alasiri na Dar leo siku iliyofuata.

Juma na Paulo walipeleka nakala ya maoni na barua kwa meya wa jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Jiji, mkuu wa mkoa na SUMATRA.

Iliamuliwa kwamba jumatatu itakayofuata Elaine angepiga simu ofisi ya meya kujua ni lini uamuzi wa mwisho utarajiwe na ikiwa maguta na mikokoteni inaruhusiwa kwenye maeneo hayo kwa wakati huu. Angejaribu pia kutafuta nakala za sheria-ndogo na mapendekezo ya marekebisho yake.

Prosper alipendekeza kuwa pamoja na kukosoa sera hii, tunatakiwa tufikirie njia nzuri itakayosaidia manispaa kupunguza msongamano barabarani.Baadhi ya mapendekezohayo ni kama vile kuwa na vyombo vya usafiri visivyotumia injini vya kutoka na kuingia katikati ya jiji kwa njia tofautitofauti,kuweka vifaa vya baiskeli kama maegesho ya baiskeli,kuongeza gharama za uegeshaji wa magari binafsi katikati ya jiji, kuweka mabasi ya kifahari yanayochukua nauli kubwa na kuimarisha sehemu za kuegesha kwa watu wenye uwezo kutumia kama mbadala wa magari binafsi (wakati huo huo kuwepo na daladala kwa wale ambao hawatakuwa tayari kutoa nauli kubwa), kuhamisha kituo cha posta na kufnya vituo vidogovidogo vitatu au vine katika maeneo tofauti ya jiji ambapo watu wataweza kutembea na kusaidia kuondoa foleni barabarani.

Ilikubalika kwamba itaandaa barua kwenda Ilala kupendekeza kuwepo na mkutano ambapo tutazungumzia pendekezo hili la kupunguza msongamano

**Msafara wa baiskeli**

Elaine alitueleza kuhusu mpango wa msafara unavyoendelea jinsi mabadiliko yalivyofanywa wiki iliyopita. Prosper alisema ataandika sehemu ya AALOCOM mapema iwezekanavyo na Elaine alisema atafuatilia kuhusu CHABADA. Baadhi ya marekebisho yalifanywa wakati wa mkutano. Elaine anasafiri kwenda Cape Town Africa ya Kusini kikazi na atajaribu kumtafuta Bradley wa ITDP. Baada ya kuwasiliana na ITDP tutaanza kutafuta wafadhili.

**Ukarabati ujao wa barabara**
Elaine aliarifu kwamba alikwenda ofisi za TANROADS Dar es Salaam wiki iliyopita na kupeleka picha za digito za mpango wa barabara za Sam Nujoma, Nelson Mandela na Kilwa. Aliziweka pia kwenye mtandao na barua pepe kuomba usaidizi wa wahandisi kutoa ufafanuzi. Alipata watu wawili waliotaka kusaidia, Robert Bartlett wa Ujerumani na Dan Piatkowski. Aliwapa maelezo na watazifanyia kazi na kutupa maelezo zaidi.

**Mengineyo**
Elaine alisema barua ya SUMATRA kama alivyoahidi lakini atakamilisha mapema iwezekanyo.

Jumanne alisema ataleta watu wengine ili wajiunge na kikundi chetu na ilipendekezwa awalete kwenye mkutano ujao ili wajaze fomu za uanachama. Pia aliomba nakala ya katiba na Elaine alisema atachapa moja kwa ajili yake.

**Mkutano ujao**
Ilikubalika kwambakukutana tena wiki mbili baadae jumamosi tarehe 28 aprili saa nne asubuhi.